

TANGAZO LA SERIKALI NA. 938 la tarehe 29/11/2019

**SHERIA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA,
(NA. 5 YA MWAKA 2019)**

AGIZO

(Imetolewa kwa mujibu wa kifungu cha 29(1)(d))

MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA KOROGWE(KOROGWE WSSA),
(BEI ZA MPITO) (MAREKEBISHO) AGIZO, 2019

Jina la Agizo

T.S. Na. 295 la
2016

1. Agizo hili litajulikana kama, Agizo la Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Korogwe(Korogwe WSSA),(Bei za Mpito) (Marekebisho), la Mwaka 2019 na litasomwa pamoja na Agizo la Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Korogwe(Korogwe WSSA),(Bei za Mpito), 2016, ambalo litajulikana kama Agizo Kuu.

Tarehe ya Kuanza

2. Marekebisho haya yataanza kutekelezwa tarehe 1 Disemba 2019 na litabakia kwenye matumizi mpaka bei mpya zitakapoidhinishwa na EWURA.

Marekebisho ya
Jedwali la Kwanza

3.-(1) Agizo Kuu itaendelea kutumika isipokuwa bei za majisafi na usafi wa mazingira zilizoainishwa kwenye Jedwali 1.3 na 1.4 al Jedwali la Kwanza.

(2) Jedwali la Kwanza linafanyiwa marekebisho kama ilivyoainishwa kwenye Jedwali katika Agizo hili.

Masharti ya
nyongeza

4. Agizo Kuu linafanyiwa marekebisho kwa kuongeza masharti ya nyongeza kwenye Agizo kuu kama ifuatavyo:

(a) ifikapo 31 Disemba 2019 au kabla, kuwasilisha mpango biashara ulioidhinishwa na Bodi ya

Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Korogwe(Korogwe Wssa), (Bei za Mpito) (Marekebisho)

TANGAZO LA SERIKALI NA.938 (linaendelea)

Korogwe WSSA;

- (b) kutekeleza masharti ambayo hayajakamilishwa utekelezaji wake katika Agizo Kuu; na
- (c) kuongeza muda wa kutoa huduma mpaka kufikia saa 12.

JEDWALI

JEDWALI LA KWANZA

MAREKEBISHO YA ADA

(Limetengenezwa chini ya aya ya 3)

Jedwali 1.3: Ada ya Sasa na Iliyoidhinishwa ya Marejesho ya Huduma ya Maji Baada ya Kukatiwa (TZS/Rejesho)

Kundi la Wateja	Ada ya Sasa	Ada Iliyoidhinishwa
Majumbani	10,000	10,000
Taasisi	10,000	10,000
Biashara	10,000	10,000
Viwanda	50,000	15,000
Magati	15,000	15,000

Jedwali 1.4: Tozo ya Huduma ya Sasana Iliyidhinishwa (Shilingi/Mwezi)

Kundi la Wateja	Ada ya Sasa	Ada Iliyoidhinishwa
Majumbani	2,000	Tozo ya Huduma Hairuhusiwi
Taasisi	2,000	
Biashara	2,000	
Viwanda	2,000	
Wateja wa Jumla na Magari ya Kuuza Maji Safi	2,000	

Dodoma
14 Novemba 2019

NZINYANGWA E. MCHANY
Mkurugenzi Mkuu